NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU
30 Desemba 2021

Kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara

Marafiki wapendwa Sana,

1. Kwenye Riḍván mwaka huu tulielezea jinsi, katika kipindi cha robo karne, ulimwengu wa Kibahá'í ulivyopitia mabadiliko ambayo yaliujalia uwezo usiowazika wa kujifunza, kukua na kuhudumia jamii ya binadamu. Lakini, hata kama mafanikio ya kipindi hiki yalikuwa yenye kuleta matumaini kiasi gani, sharti yafunikwe na yale yanayokuja. Kwa hitimisho la mfuatano mpya wa Mipango iliyoanza hivi karibuni, jumuiya ya Kibahá'í itahitaji kuwa imejipatia uwezo ambao kwa wakati huu unaweza kuonekana kidogo sana. Katika mashauriano yenu ya kina ya siku zijazo, mtakuwa mkijishughulisha na kuchunguza kile kinachohitajika kuileta kwenye uwepo jumuiya iliyoimarishwa kama hiyo.

2. Bahá'u'lláh husema kwamba "kusudi ambalo kwalo watu wa umauti, kutoka katika hali ya kutokuwepo kabisa, wameweza kuingia katika milki ya uwepo, ni kwamba waweze kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu na kuishi pamoja kwa mapatano na maelewano." Yeye Amefunua mafundisho ambayo hulifanya hili liwezekane. Ujengaji jamii ambayo kwa kutambua hushughulikia kusudi hili la pamoja siyo kazi ya kizazi hiki pekee, bali ya vizazi vingi vijavyo, na wafuasi wa Bahá'u'lláh huwakaribisha wote ambao hujishughulisha pamoja nao katika jitihada hii. Humaanisha kujifunza jinsi ya kuibua jumuiya zilizoshamiri, zenye mtazamo wa nje; humaanisha jumuiya hizo kujifunza jinsi ya kuleta maendeleo ya kiroho na kimwili; humaanisha kujifunza jinsi ya kuchangia katika midahalo ambayo huathiri muelekeo wa maendeleo hayo. Maeneo haya ya jitihada, kwa kawaida, ni yale yanayofahamika. Yakitazamwa katika muono mmoja, yapo tofauti kabisa, kila moja likiwa na sifa zake bainifu lenyewe na mambo ya kuzingatia. Walakini yote yanawakilisha njia za kuamsha nguvu zilizofichika katika roho ya mwanadamu na kuzielekeza kwenye uboreshaji wa jamii. Kwa pamoja, ni njia za kuachilia kile ambacho Mlinzi alikieleza kama "nguvu ya Imani ya ujengaji jamii". Nguvu hii iliyomo katika Hoja ya Bahá'u'lláh inaonekana hata katika jitihada changa za jumuiya ya Kibahá'í inayojifunza kuhudumia jamii ya binadamu na kuendeleza Neno la Mungu. Na ingawa jamii ya ulimwengu inayofunikwa na Ufunuo Wake ipo bila shaka mbali sana, jumuiya zinazojifunza kwa shauku kuweka mafundisho Yake katika uhalisia wao wa kijamii ni nyingi. Ni kwa kiasi kikubwa jinsi gani zimebarikiwa zile roho ambazo, zikitambua ukuu wa Siku hii na umuhimu wa vitendo vyao, huweka jitihada kwa ajili ya uibukaji wa jamii inayobumbwa na mafundisho matakatifu.

3. Mfuatano wa Mipango ya kiulimwengu ambayo ilianza Riḍván utadumu kwa miaka ishirini na tano kamili. Utaibeba safina ya Hoja kuelekea karne ya tatu ya Zama za Kibahá'í na kuhitimishwa mnamo Riḍván 2046. Katika kipindi hiki, ulimwengu wa Kibahá'í

utamakinikia kwenye shabaha moja: uachiliaji wa nguvu ya Imani ya ujengaji jamii kwa viwango vikubwa daima. Utekelezaji wa lengo hili la jumla utahitaji uinukaji zaidi katika uwezo wa muumini binafsi, jumuiya ya mahali na asasi za Imani. Wahusika hawa wakuu watatu wa kudumu wa Mpango kila mmoja ana sehemu inayomhus, na kila mmoja ana uwezo na sifa ambazo sharti zikuzwe. Hata hivyo, kila mmoja hawezi kudhihirisha uwezo kamili peke yake. ‘Ni kwa kuimarisha uhusiano wao wa nguvu mmoja kwa mwingine kwamba nguvu zao zinaunganishwa na kuzidishwa. ‘Abdu’l-Bahá hueleza kwamba kadiri sifa za ushirikiano na kusaidiana zinavyodhihirishwa na kundi la watu, “ndivyo zaidi jamii ya binadamu itakavyosonga mbele katika maendeleo na kushamiri”; katika Imani, kanuni hii hutofautisha na kutengeneza maingiliano ya watu binafsi, asasi na jumuiya, na hulijalia umbo la Hoja nguvu ya kimaadili na afya ya kiroho.

4. Roho zilizowashwa zikiinuliwa kupitia michakato ya Mpango zinatafuta daima kupata uelewa wa kina wa mafundisho ya Bahá’u’lláh—“tiba yenye mamlaka ya kila ugonjwa”— na kuyatumia kwa mahitaji ya jamii yao. Zimejidhatiti kwa ajili ya ushamiri wa wote, zikitambua kwamba ustawi wa watu binafsi umo kwenye ustawi wa jamii kwa ujumla. Wao ni raia watiifu ambao huepuka kushiriki katika vyama vya siasa na kugombea vyeo vya kidunia. Badala yake, wanamakinikia kuzishinda tofauti, wakiweka pamoja mitazamo, na kukuza matumizi ya ushauriano katika kufanya maamuzi. Wanasisitiza sifa na mitazamo—kama vile uaminifu, ushirikiano na ustahimilivu—ambazo ni zana kwa ajili ya ujengaji wa utaratibu usioyumba wa kijamii. Wanatetea urazini na sayansi kama muhimu kwa ajili ya maendeleo ya jamii ya binadamu. Wanasimamia ustahimilivu na maelewano, na wakiweka juu kabisa katika fikra zao asili ya umoja wa jamii ya binadamu, wanamuona kila mmoja kama mdau muhimu wa kushirikiana naye, na wanafanya juhudi kuendeleza hisia ya kirafiki hata baina ya makundi ambayo kwa jadi yamekuwa na uhasama moja kwa jingine. Wanatambua jinsi nguvu za uyakinifu na anasa za kidunia ziwazungukazo zinavyofanya kazi, na macho yao yapo wazi kabisa kwa udhalimu mwingi unaoendelea ulimwenguni, bado wana mtazamo sahihi juu ya nguvu ya ujengaji ya umoja na uwezo wa jamii ya binadamu kuwafikiria wengine kuliko nafsi. Wanaona nguvu iliyomo katika dini ya kweli katika kubadili mioyo na kushinda kutoaminiana, na hivyo, wakiwa na imani katika kile ambacho kimo katika siku za usoni, wanafanya jitihada kulea hali ambamo maendeleo yaweza kutokea. Wanashiriki imani zao na wengine kwa ukarimu, wakiwa wenye kuheshimu uhuru wa mawazo ya kila roho, na hawashinikizi vipimo vyao kwa yeyote. Na wakati wasingejifanya kuwa wamegundua majibu yote, wanatambua dhahiri juu ya kile walichojifunza na kile ambacho bado wanahitaji kujifunza. Juhudi zao husonga mbele kwa mdundo wa kupokezana wa vitendo na tafakari; vikwazo haviwasumbui. Katika maeneo ambako idadi zikuazo zinasaidia kujenga jumuiya za aina hii, nguvu ya Hoja ya kubadili maisha ya watu kijamii, vile vile maisha yao ya ndani, inatokea kuwa wazi zaidi na zaidi. Shauku ya utekelezaji wa shabaha kuu ya Mpango, tuna hakika, itasababisha kuibuka kwa jumuiya kama hizi nyingi zaidi na zaidi.

***Mjongeo wa klasta***

5. Muonekano mkubwa zaidi wa nguvu ya Imani ya ujengaji jamii huhitaji, kwanza na muhimu kabisa, bado uendelezaji zaidi wa mchakato wa uingiaji kwa makundi katika kila sehemu ulimwenguni. Wajibu wa kimsingi wa kiroho wa kueneza mwanga wa Ufunuo wa Bahá’u’lláh daima kwa mapana zaidi na kueneza mizizi ya Imani Yake kwa kina zaidi

katika udongo wa jamii una matokeo yanayopimika: idadi ya klasta ambamo programu ya ukuaji imeanzishwa na kiwango cha ushadidi ambacho kila moja imekifikia. Nyenzo sasa zipo kwa ajili ya kupiga hatua ya haraka kuhusiana na vipimo vyote viwili. Lengo ambalo jumuiya ya Jina Kuu Kabisa sharti linuie kulitimiza katika mfuatano wa sasa wa Mipango ya ulimwengu ni kuanzisha programu za ukuaji shadidi katika klasta zote ulimwenguni. Lengo hili kuu kabisa humaanisha upanuzi na ushadidishaji wa shughuli katika kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa. Maendeleo ya haraka kuelekea lengo hili lazima yafikiwe katika kipindi cha Mpango wa Miaka Tisa.

6. Kama hatua ya awali, tunaomba kwamba muyasaidie Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na Halmashauri za Kibahá'í za Kanda kuamua ikiwa mipango yao ya kugawanya maeneo yao katika klasta itanufaika kutokana na marekebisho yoyote. Kama mjuavyo, klasta huelezea eneo ambako shughuli za Mpango zinaweza kuchochewa kwa njia inayoweza kusimamiwa na kudumishwa. Katika miaka ishirini na moja iliyopita, ujifunzaji mwingi umepatikana kuhusu ukubwa wa klasta ambao unaweza kusimamiwa katika muktadha mbalimbali na katika sehemu mbalimbali za ulimwengu; katika baadhi ya nchi, marekebisho tayari yameanza kufikiriwa, yakitokana na athari za ukuaji. Katika hali nyingi tathmini hii mpya haitaleta mabadiliko yoyote, lakini kwa baadhi itasababisha klasta kugawanywa ama kupunguzwa ukubwa, na kwa nadra klasta inaweza kuwa kubwa zaidi. Maeneo ambayo yana watu waliotawanyika kutokana na jiografia ya eneo yanaweza kuenguliwa katika mfumo wa klasta. Bila shaka, waumini wowote ambao huishi katika maeneo kama hayo wangeweza kutwaa vipengere vingi iwezekanavyo vya muundo wa utendaji kama ufaavyo kutumika katika mazingira yao.

7. Mjongeo wa klasta katika mwendelezo wa maendeleo utaendelea kuwa mtindo wa msingi wa upanuzi na uimarishaji wa jumuiya. Sifa bainifu za njia ya maendeleo ambayo inabidi ifuatwe, na hususan katika hatua za kwanza, pili na tatu za ukuaji ambazo huonesha upigaji hatua katika njia, tayari zinajulikana vizuri kwa marafiki kutoka jumbe zetu zilizopita na kutoka tajiriba yao wenyewe, na hatuhisi haja ya kurudia kile tulichosema huko nyuma. Hadi kufikia mwisho wa Mpango wa Mwaka Mmoja tunatazamia kuwa programu za ukuaji zitakuwa zinakaribia klasta 6,000, kwamba takribani 5,000 ya hizi zitakuwa zimepita hatua ya pili ya ukuaji, na kwamba kati ya 1,300 ya hizi waumini watakuwa wamesonga mbele zaidi. Takwimu hizi lazima zipande sana katika kipindi cha miaka tisa ijayo. Mara marekebisho yoyote kwenye mfumo wa klasta yametambulika katika kila nchi, tunaomba kwamba mfanye kazi na Mabaraza ya Kitaifa na Halmashauri za Kanda kukadiria idadi za klasta ambako huenda maendeleo yatafanywa kuvuka hatua ya kwanza, ya pili na ya tatu ya ukuaji, mtawalia, wakati wa Mpango. Ikumbukwe kwamba haya yanakusudiwa tu kuwa makadirio ya taarifa sahihi; yanaweza kuboreshwa baadaye kadiri itakavyohitajika na hayahitaji kufanyiwa kazi kwa muda mrefu. Na hivyo, tunaomba kwamba matokeo ya tathmini hizi yatumwe Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu ifikapo Naw Ruz. Hapo ifikapo Riḍván, tutaweza kutoa matarajio ya jumla ya Ulimwengu wa Kibahá'í kwa ajili ya Mpango wa Miaka Tisa.

8. Tunatambua kwamba kuna baadhi ya kanda na nchi ambako Imani imebaki katika hatua ya awali ya ukuaji, na kuna hitaji la haraka kuhakikisha kwamba kile ambacho ulimwengu wa Kibahá'í umejifunza kuhusu uchapuzaji wa mchakato wa ukuaji huyanufaisha maeneo haya pia. Somo moja muhimu ambalo limekuwa wazi ni thamani

kubwa kwa kanda, yenye klasta ambayo imevuka hatua ya tatu ya ukuaji. Mara marafiki katika klasta fulani wamekuza uwezo mbalimbali ambao kwao maendeleo kama hayo humaanisha, na mbinu za kusambaza umaizi na kushirikiana tajiriba kuhusu jitihada za ujenzi wa jumuiya zipo, basi uchapuzwaji wa haraka wa shughuli za upanuzi na uimarishaji katika klasta zinazoizunguka huwezekana. Tukiwa na hili akilini, ni muhimu sana kwamba katika kipindi cha Mpango wa Miaka Tisa mchakato wa ukuaji ufikie kiwango hiki cha nguvu katika walau moja ya klasta katika kila nchi na kila kanda. Hii hujumuisha moja ya malengo makuu ya Mpango na itahitaji juhudi makinifu za roho nyingi zilizojiweka wakfu. Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa kipo tayari kufanya kazi nanyi katika kutekeleza mikakati kadhaa katika kulifikia hili. Muhimu kabisa miongoni mwa haya itakuwa ni utumaji wa timu za watangulizi wa kimataifa na wa nyumbani ambao wana ufahamu wa muundo wa utendaji na wamejiandaa kutoa kiasi cha kutosha cha muda na nguvu katika kuhudumia Hoja kwa miaka kadhaa. Mtahitaji kuyavutia Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na Halmashauri za Kibahá′i za Kanda juu ya uharaka wa kuwatia moyo waumini ambao, wakifuata nyayo za roho nyingi sana za kishujaa za wakati uliopita, wanaweza kuinuka kuhakikisha kwamba mwanga wa Imani huwaka kwa wangavu katika kila eneo. Tunatazamia hususan kwenye nchi, kanda na klasta ambamo nguvu na tajiriba vimekusanywa kuzalisha mtiririko wa watangulizi kwenda kwenye maeneo ambako msaada unahitajika, na pia kutoa usaidizi kwa namna nyinginezo. Mtiririko huu wa usaidizi ni njia mojawapo zaidi ambamo moyo wa ushirikiano na kusaidiana, ambavyo ni muhimu sana kwa maendeleo, hujidhihirisha vyenyewe katika utendaji wa mpangilio.

9. Mafanikio ya mfuatano uliopita wa Mipango—hususan Mpango wa mwisho wa Miaka Mitano—yasingeweza kupatikana bila kupiga hatua kubwa katika shughuli za ufundishaji. Kipimo muhimu cha kazi hii ni uwezo wa kujihusisha katika mazungumzo juu ya dhima za kiroho, uwezo ambao ulichunguzwa katika ujumbe wetu kwenye kongamano lenu la 2015, ambapo tulielezea jinsi gani unavyokuzwa kupitia ushiriki katika kozi za taasisi na kwa kupata tajiriba ya kivitendo. Ni dhahiri kwamba mtindo wa shughuli unaokunjuka katika ngazi za umma hufungua mazingira tofauti tofauti ambamo roho pokevu—wakati mwingine familia nzima au kundi-rika—wanaweza kushiriki katika mazungumzo ya maana ambayo huamsha shauku ya muono wa Imani na Nafsi ya Bahá′u′lláh. Baada ya muda, roho nyingi kama hizi huanza kujtambulisha zenyewe na jumuiya ya Kibahá′i, hasa kadiri zipatavyo ujasiri wa kushiriki katika maisha ya jumuiya kupitia huduma. Bila shaka, jumuiya hukaribisha kiwango chochote cha ujihusishaji ambacho mtu angependa kukidumisha, kiwe kikubwa au kidogo. Bado kumtambua Bahá′u′lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu na kupata manufaa na majukumu ambayo kipekee yanahusiana na ufuasi katika jumuiya ya Kibahá′i ni tukio moja katika maendeleo ya kiroho ya mtu, tofauti kabisa kutoka ushiriki wa mara kwa mara katika shughuli za Kibahá′i au kuunga mkono kanuni za Kibahá′i. Tajiriba imeonesha kwamba mazingira yaliyotengenezwa na jitihada za ujengaji wa jumuiya katika eneo humwezesha yeyote anayependa kupiga hatua hii kufanya hivyo kwa urahisi zaidi. Popote ambapo jitihada hizi zinaendelea, ni muhimu kwa marafiki kuwa makini kwamba milango ya Imani ipo wazi kabisa na kuwatia moyo wale ambao husimama kizingitini. Na katika maeneo ambako jitihada kama hizo zimeanzishwa vyema kwa muda fulani, waumini wengi wanagundua kwamba mtindo wa shughuli wenye nguvu, upanukao kwa kawaida unaweza kusababisha familia, makundi ya marafiki, na hata makundi ya kaya kadhaa kuwa tayari kuingia katika Hoja. Kwani katika maeneo yenye fursa ambapo uwezekano wa kujiunga na jumuiya unaweza kujadiliwa kwa uwazi

na kwa pamoja miongoni mwa wale ambao hushiriki hisia ya utambulisho wa pamoja, roho zinaweza kujihisi kutiwa ujasiri kwa urahisi zaidi kupiga hatua hii kwa pamoja. Asasi za Kibahá'í, hasa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali, lazima yawe na fikra ambayo huruhusu maendeleo kama hayo, na kuhakikisha kwamba vikwazo vyote vimeondolewa.

10. Tunawaomba ninyi na wasaidizi wenu kuwasaidia waumini, popote waishipo, kutafakari mara kwa mara juu ya njia zifaazo za ufundishaji wa Imani katika vyao vyao, na kuchochea ndani ya mioyo yao shauku kwa ajili ya ufundishaji ambayo itavuta mathibitisho ya Ufalme Mtakatifu. Roho ambazo zimepewa baraka ya imani zina shauku ya kawaida ya kushiriki zawadi hii kupitia mazungumzo na ndugu, marafiki, wanafunzi wenza, wafanyakazi wenza na wale ambao hawakuwahi kukutana nao kabla, wakitafuta kila mahali na kila wakati sikio sikivu. Mazingira na hali tofauti hujipelekea zenyewe kwenye mbinu tofauti, na marafiki wanapaswa wajishughulishe katika mchakato unaoendelea wa ujifunzaji kuhusu kile ambacho ni chenye ufanisi zaidi pale waishipo.

***Ujifunzaji kutoka klasta zilizopiga hatua zaidi***

11. Miaka sita iliyopita tuliwaelezea sifa ya klasta ambayo marafiki wamepita hatua ya tatu ya ukuaji kwenye muendelezo wa ukuaji. Kuweza kufika hapa humaanisha shughuli shadidi inayotokea katika ujirani au vijiji mahususi, lakini pia jitihada makinifu zinazofanywa na waumini wote waishio katika klasta nzima—kwa maneno mengine, moyo unaoinuka wa ushiriki wa wote katika kazi ya ujenzi wa jumuiya. Kiutendaji, hii humaanisha kuhamasisha idadi ya kutosha ya Wabahá'i wanaotumia muundo wa utendaji wa Mpango kiubunifu na kiakili kwenye uhalisia wa mazingira yao wenyewe popote waishipo kwenye klasta. Hujumuisha familia na waumini binafsi kufanya kazi kwa pamoja na kufanya uamuzi makini kujiona wenyewe kama sehemu ya kiini kipanukacho. Makundi kama hayo ya marafiki hujiingiza katika upanuzi wa duara la ushiriki katika shughuli zao kwa kujihusisha na mitandao ambayo wao ni sehemu yake—mitandao iliyoundwa kupitia mahali pa kazi au masomo, shule ya eneo hilo, au kiunganishi cha jumuiya cha aina nyingine—na kwa kuambatana na wengine ambao huinuka kuhudumu pamoja nao. Juhudi hizi zina manufaa makubwa. Hata pale ambapo klasta inayo idadi ya vituo vinavyoshamiri vya shughuli shadidi, jitihada zinazofanywa kwingineko katika klasta bado zinaweza kuwakilisha idadi kubwa ya shughuli zote zinazoendelea. Kuhusiana na hii, pia tunatambua, hatua zinazochukuliwa katika baadhi ya klasta kuwafikia kimpangilio idadi fulani ya watu ambayo imeonesha upokevu kwa Imani lakini imesambaa katika klasta nzima. Hii inaweza kuonekana kama muundo mahususi wa kazi ya ujengaji jumuiya, na moja ambayo huendelea kuonesha matumaini makubwa. Kadiri ushiriki katika kazi ya Mpango katika miundo yake yote uongezekavyo, fursa nyingi huibuka kwa marafiki kujifunza kutoka tajiriba ya kila mmoja na kuwasha ndani ya kila mmoja furaha ya ufundishaji.

12. Bila shaka, shughuli inayofanyika katika ujirani na vijiji vyenye upokevu imekuwa shabaha maalum ya umakinifu katika miaka ya hivi karibuni. Kadiri wakazi wa maeneo kama hayo wanavyoanza kushiriki katika shughuli za Kibahá'í kwa idadi kubwa, umakini zaidi huhitajika kutolewa ili kuendana na utata wa kiasili unaohuska. Ndani ya kila kituo chenye shughuli shadidi, mipangilio shirikishi huibuka miongoni mwa makundi ya familia, ambao huandaa shughuli za ujengaji jumuiya miongoni mwao wenyewe wakiwa na

mtazamo wa kupanua ukumbatiaji wa shughuli kama hizo kwa kaya nyingi za karibu karibu; mtandao usio rasmi wa marafiki hutoa hamasa na usaidizi wa jitihada zinazoendelea. Mwenendo wa maisha ya kila siku katika maeneo kama haya unajiambatanisha na uibukaji wa utamaduni ambao ibada na huduma ni shughuli zinazothaminiwa zikijumuisha watu wengi kwa wakati mmoja. Mikusanyiko ya kusisimua ya jumuiya, iliyoandaliwa vyema—katika baadhi ya hali hadi kufikia kambi na matamasha—hutokea mara kwa mara zaidi, na muziki na nyimbo hutokeza kwa kiwango cha juu kwenye matukio kama haya. Kwa hakika sanaa kwa jumla, sehemu muhimu sana katika maendeleo ya jumuiya tangu mwanzoni, hujitokeza kipekee katika mazingira kama hayo kama njia muhimu ya kuchochea furaha, kuimarisha mafundo ya umoja, kusambaza maarifa na kuimarisha uelewa, na vile vile kuwafahamisha wale wa jamii pana zaidi kuhusu kanuni za Hoja. Na kwa kawaida, hapo unabakia msisitizo wa kuwa kwenye mtazamo wa nje: tukitafuta njia za kuendelea kushiriki matunda ya ruwaza inayoshamiri ya utendaji pamoja na roho ambazo bado haziifahamu Imani.

13. Katikati ya haya yote, tumebaini jambo moja maalum, linalotia moyo, ambalo vidokezo vyake vya awali tulivielezea katika ujumbe wetu kwenye kongamano lenu la 2015 kama linalowakilisha wigo mpya. Ingawa kujifunza jinsi ya kukumbatia idadi kubwa ni sifa bainifu ya klasta yoyote ambako hatua ya tatu ya ukuaji imevukwa, umakinikiaji wa marafiki kwa ulazima huanza kupanuka kadiri wakaribiapo mahali ambapo uwiano wa maana wa idadi ya watu katika eneo fulani inashiriki katika shughuli za ujenzi wa jumuiya. Hii inaweza kuwa kweli kwa eneo maalum tu la makazi ndani ya klasta, au kwa maeneo kadhaa kama hayo, au kwa kijiji kimoja; sehemu zingine za klasta zinaweza kuwa bado kushiriki uhalisia huu. Lakini katika maeneo kama hayo, fikra za marafiki wanaofanya kazi kwenye ngazi ya umma huendelea kujihusisha na maendeleo na ustawi wa kila mmoja anayeishi katika viunga vyake. Asasi za Kibahá'í hujisikia kuwa makini zaidi katika wajibu wao kwa ajili ya elimu ya kiroho ya kizazi kizima cha watoto na vijana chipukizi, wengi wao ama hata kwa ujumla wao tayari wanaweza kuwa wanajihusisha katika shughuli za jumuiya. Mabaraza ya Mahali huimarisha uhusiano wao na mamlaka na viongozi wa mtaa, hata kuingia katika ushirikiano rasmi, na umakini unaokua hutolewa kwa ubunifu unaoongezeka wa jitihada za jamii uibukao kutoka vikundi vya vijana chipukizi, vijana, wanawake, familia, au wengine wanaoitikia mahitaji yanayowazunguka. Kuwa kwenye ngazi hiyo na shughuli mbalimbali huhitaji Washauri Wasaidizi kuteua wasaidizi wengi kuhudumu katika kijiji au ujirani mmoja; kila msadizi aweza kufuatilia njia moja au zaidi ya utendaji, akitoa ushauri na usaidizi kadiri ihitajikavyo, na kutoa msukumo katika michakato iliyo katika mwendo.

14. Katika maeneo ambako shughuli za Mpango zimefikia kiwango kama hicho cha ueneaji, wakazi sasa huwa na uwezo uliongezeka vya kutosha kuongoza njia ya maendeleo yao wenyewe, na asasi pamoja na mawakala wa Imani hapo sasa huwa na mtazamo mpana wa wajibu wao. Bila shaka, wajibu huu bado hujumuisha kuwa na mifumo imara ili kuendelea kujenga uwezo na kuwasaidia wale wanaochukua hatua. Lakini maendeleo ya jumuiya hutegemea, kwa kiwango kikubwa kuliko hapo awali, juu ya asasi za mahali na mawakala kuwa na ufahamu wa nguvu za kijamii zinazofanya kazi katika mazingira na wakitenda kuhifadhi uadilifu wa jitihada nyingi za jumuiya.

Wakati huo huo, uhusiano wa jumuiya ya Kibahá'í na jamii inayowazunguka hupitia mabadiliko ya kina. Kama inavyowakilishwa na miundo yake rasmi ya kiutawala na mipangilio isiyo rasmi ya kiushirikiano, jumuiya ya Kibahá'í imekuwa ni mdau mkuu anayeonekana vizuri zaidi katika jamii kwa nafasi yake yenyewe, ile ambayo ipo tayari kubeba majukumu muhimu na kushadidisha mchakato mpana wa ujifunzaji wa pamoja juu ya maendeleo ya kiroho na ya kimwili. Wakati huo huo, kadiri jamii pana zaidi ikumbatiavyo vipengele vingi vya maisha ya jumuiya ya Kibahaí na kusharabu kutoka roho yake iunganishayo, nguvu zinazojengwa hivyo huruhusu makundi anuwai kuja pamoja katika mjongeo ulionganishwa ukivuviwa na muono wa Bahá'u'lláh wa umoja wa jamii ya binadamu. Here is witnessed a release of the society-building power of the Faith unlike anything that has been seen before. Hii leo, idadi ya maeneo ambayo mtindo wa maisha ya jumuiya ya Kibahá'í umefikia ueneaji huo ni ya wastani, lakini inaendelea kukua. Hapa unashuhudiwa uachiliwaji wa nguvu ya Imani ya ujengaji jamii ambayo haifanani na chochote kilichowahi kuonekana hapo kabla.

15. Kwa kawaida, ueneaji wa hughuli ya Kibahá'í kwa kiwango hiki siyo matarajio ya kila mahali. Ni muhimu kukubali tofauti inayotengenezwa na hali ndani ya klasta au katika sehemu ya klasta na kwa mienendo ya kundi la watu—yaani, kutokana na uhalisia wa mazingira. Kimantiki, njia ambamo nguvu ya Imani ya ujengaji jamii itajionesha katika mazingira tofauti zitatofautiana. Lakini bila kujali kiwango ambacho maisha ya jumuiya ya Kibahá'í huwakumbatia wale ambao huishi katika eneo fulani— bila kujali, hata ushadidi wa programu ya ukuaji katika klasta au kiwango cha shughuli katika ujirani au Kijiji—changamoto inayowakabili marafiki wanaohudumu kwenye ngazi ya umma kimsingi ni ile ile kila mahali. Lazima wawe na uwezo wa kusoma uhalisia wao wenyewe na kuuliza: ni yapi, kutokana na uwezekano na mahitaji tuliyonayo, yangekuwa malengo yafaayo kutekelezwa katika duru au mfuatano wa maduru yajayo? Ninyi pamoja na wasaidizi wenu mpo katika nafasi nzuri kuuliza swali hili na kuhakikisha kwamba mikakati inayofaa inatambuliwa. Mafunzo mengi yanaweza kupatikana kutokana na tajiriba ya marafiki katika klasta zinazofanana, kwa jumuiya iliyo hatua moja mbele zaidi kwenye njia hiyo hiyo inaweza kutoa umaizi wenye thamani juu ya lengo lifuatalo la kupambania. Kadiri marafiki wanavyotafakari kwa kina juu ya kile kilichopo mbele yao, wataweza kuona kwa urahisi kwamba kwa kila jumuiya kuna lengo la kufikika, na kwa kila lengo njia ya kulifikia. Tukiwa tunaangalia mbele katika njia hii, je, tusingeweza kumuona Bahá'u'lláh Mwenyewe, hatamu za masuala ya jamii ya binadamu katika mkono mmoja, mkono Wake mwingine ukiwaita wote harakisheni, harakisheni?

***Uchangiaji kwa mabadiliko ya kijamii***

16. Ufunuo wa Bahá'u'lláh unahusiana na mabadiliko yote mawili ya maisha ya ndani ya mwanadamu na mazingira ya kijamii. Barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi huelezea jinsi mazingira ya kijamii hutoa "hali" ambamo mioyo yaweza "kukua kiroho na kuakisi kikamilifu mwanga wa Mungu" ungáao kupitia Ufunuo. Ishara dhahiri kwamba nguvu ya Hoja ya ujengaji jamii inaachiliwa katika klasta ni kwamba juhudi zinafanywa na idadi ikuayo ya wakazi wake, wakivuviwa na mafundisho ya Imani, kusadia kuboresha hali ya kiroho na hali za kijamii za jumuiya pana zaidi ambamo wao

ni sehemu yake. Mchango unaofanywa na Wabahá'í hutofautishwa kwa msisitizo wake juu ya ujengaji uwezo kwa ajili ya huduma; ni mbinu ambayo hutokana na imani katika uwezo wa kundi la watu ili wawe wadau wakuu wa maendeleo yao wenyewe.

17. Kadiri ushadidi wa kazi ya ujengaji jumuiya uongezekavyo katika klasta, hapo marafiki bila kuepuka huwa na utambuzi zaidi wa vikwazo vya kijamii, kiuchumi au kitamaduni ambavyo vinazuia maendeleo ya kiroho na kimwili. Watoto na vijana chipukizi wanaokosa usaidizi katika elimu yao, shinikizo kwa wasichana litokanalo na desturi za kitamaduni zinazohusiana na ndoa za utotoni, familia zikihitaji msaada kupita katika mifumo wasiyoifahamu ya huduma ya afya, kijiji kinachohangaikia kupata baadhi ya mahitaji ya msingi, au chuki iliyodumu kwa muda mrefu itokanayo na uhasama uliorithiwa kati ya makundi tofauti—wakati juhudi za jumuiya ya Kibahá'í katika nyanja ya upanuzi na uimarishaji huzikutanisha na hali hizi na nyingine nyingi, itavutwa kuitikia kwenye uhalisia kama huo kadiri mazingira yake yanavyoruhusu. Katika kutafakari juu ya hali kama hizo inakuwa dhahiri kwamba, ndani ya klasta, upanuzi na uimarishaji, shughuli za kijamii, na uchangiaji katika mijadala inayoendelea ni vipengele vya jitihada moja, iliyounganishwa, yenye mtazamo wa nje inayotekelezwa kwenye ngazi ya umaa ya jamii. Jitihada zote hizi hufanyika kulingana na muundo wa pamoja wa kiutendaji, na hili juu ya mengine yote huleta mwambatano kwenye mtindo wa jumla wa shughuli.

18. Vichocheo vya awali vya shughuli za kijamii kwenye ngazi ya umma huanza kuonekana katika klasta kadiri upatikanaji wa rasilimali watu unavyoongezeka na uwezo kwa ajili ya uwanda mpana wa majukumu unavyokua. Vijiji vimethibitisha kuwa maeneo yenye rutuba kabisa ambayo kwayo jitihada za shughuli za kijamii zimeibuka na kudumishwa, lakini vile vile katika maeneo ya mjini, marafiki wanaoishi huko wamefanikiwa katika kutekeleza shughuli na miradi inayofaa kwa mazingira ya kijamii, wakati mwingine kwa kufanya kazi na shule za maeneo hayo, mawakala wa asasi za kiraia, au hata na vyombo vya kiserikali. Shughuli za kijamii zinafanyika katika nyanja kadhaa muhimu, zikiwemo mazingira, kilimo, afya, sanaa, na hasa elimu. Katika kipindi cha Mpango wa Miaka Tisa, na hasusani kadri usomaji wa kozi mahususi za taasisi unavyochochea shughuli kuu zaidi katika nyanja hii, tunatarajia kuona ueneaji wa jitihada rasmi na zisizo rasmi za kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya kundi la watu. Baadhi ya jitihada hizi kwenye ngazi ya jumuiya zitahitaji kuwepo kwa miundo ya kimsingi ya kiutawala ili kudumisha kazi zake. Pale ambapo hali huridhisha, Mabaraza ya Kiroho ya Mahali yatahitaji kutiwa moyo kujifunza jinsi ya kulea vizuri zaidi jitihada mpya, changa na kuendeleza jitihada zinazoonesha matumaini. Katika baadhi ya hali, mahitaji yanayoendana na nyanja maalum ya jitihada yatahitaji uanzishwaji wa mashirika yenye uvuvio wa kibaha'i, na tunatazamia uibukaji zaidi wa mashirika kama hayo katika Mpango ujao. Kwa upande wao, Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa yatalazimika kutafuta njia ambazo kwazo yatabakia yenye kufahamishwa vyema juu ya mafunzo yanayopatikana kwenye ngazi ya umma ya jumuiya zao na kuchambua tajiriba inayopatikana; katika baadhi ya maeneo hili litahitaji uundwaji wa chombo kilichojidhatiti kufuatilia shughuli za kijamii. Tunapoangazia katika ulimwengu mzima wa Kibahá'í, tunafurahishwa kuona ni kiasi gani cha kasi tayari kimeanziwa katika eneo hili la jitihada kupitia utiaji moyo na usaidizi wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Kibahá'í.

19. Unaohusiana kwa karibu na uwezo wa kushiriki katika shughuli za kijamii ni uwezo wa kuchangia katika mijadala ya kijamii. Moyoni, huu kimsingi ni uwezo wa kushiriki katika mazungumzo maalumu kwenye mada zinazogusa maisha ya watu na kutoa mtazamo unaotokana na kanuni za Kibahá'í na tajiriba ya Kibahá'í. Ikiangaliwa kwa namna hii, ni ujuzi ambao Wabahaí wengi wanapata fursa ya kujizoeza takribani kila siku, mathalani katika masomo yao au kazi zao, na ambao hulelewa kwa kushiriki kwenye kozi za taasisi; katika hali yake ya muonekano rasmi zaidi, ni msingi kwa kazi ya Jumuiya ya Kibahá'í ya Kimataifa na Ofisi za kitaifa za Mambo ya Nje. Hata hivyo, kuhusiana na uachiliaji wa nguvu ya Imani ya ujengaji jamii kwenye ngazi za umma, ni uwezo ambao huja kuwa hitaji kubwa zaidi kadiri ujihusishaji wa karibu zaidi na idadi ya watu, walioletwa kupitia kazi ya upanuzi na uimarishaji, husababisha uongezekaji wa utambuzi wa matatizo ya kijamii yaliyopo kwenye eneo, vile vile na wa shauku ya watu wake kuondokana nayo. Kadiri idadi ya wale wanaoshiriki katika shughuli za ujengaji jumuiya inavyoongezeka, ndivyo jinsi hitaji la jumuiya ya Kibahá'í kutoa, kama chombo kilichounganika, mtazamo ilionao juu ya vikwazo kwa maendeleo ya kijamii na juu ya masuala ambayo huelemea akili na mioyo ya wale inaochangamana nao. Hii ina athari maalum kwa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali. Katika maeneo ambako shughuli za Mpango zimefikia kiwango cha kuenea, Baraza huanza kutazamwa kwa mapana zaidi kama chanzo cha umaizi wa kimaadili. Baada ya muda, jitihada za kuchangia katika mijadala ya kijamii huwa zenye mpangilio zaidi, na Wabahaí huwiwa kusaidia wale wanaowazunguka kujihusisha kwa namna inayojenga katika mijadala na kufikia muafaka. Fursa hutafutwa kushiriki mtazamo wa Imani na viongozi wa jumuiya na watu walio katika mamlaka, na nafasi hutengenezwa ambapo wawakilishi wa makundi na maslahi mbalimbali wanaweza kusadiwa kufikia mtazamo wa pamoja kupitia ushauriano. Tunafurahishwa na hatua ambazo tayari zimekwishachukuliwa kujifunza jinsi umaizi kutoka Ufunuo wa Bahá'u'lláh na kutokana na tajiriba ya jumuiya za Kibahá'í vinavyoweza kutumika kusaidia masuala yanayoisumbua jamii kwenye ngazi ya mahali; mengi zaidi katika suala hili kwa hakika yanatarajiwa kufunzwa katika kipindi cha Mpango wa Miaka Tisa.

20. Tunapenda kusisitiza kwamba, kihistoria na sasa, shughuli za kijamii na jitihada za kushiriki katika mijadala iliyosambaa ya kijamii zimeibuka siyo tu katika muktadha wa ukuaji, bali pia kama matokeo ya Wabahá'í binafsi wakijitahidi kuchangia kwenye maendeleo ya jamii kwa njia zilizo mbele yao. Kama muitikio binafsi kwa miito ya Bahá'u'lláh ya kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu, waumini kwa namna mbalimbali wamechagua kufanya aina fulani ya kazi za kitaalam na wametafuta fursa kuunga mkono shughuli za makundi na mashirika yenye fikra zinazofanana. Miradi, yote mikubwa na midogo, imeanzishwa ili kuitikia kwenye masuala mbalimbali ya kijamii. Mashirika kadhaa yenye uvuvio wa Kibahá'í yameanzishwa na makundi ya watu binafsi ili kuyafanyia kazi malengo mengi tofauti tofauti, na vyombo vya kitaalamu vimeasisiwa ili kutoa umakinifu kwenye mjadala mahususi. Jitihada zote hizi, kwenye kiwango chochote kile cha utekelezaji, zimenufaika kutokana na kuwa na uwezo wa kuchota kwenye kanuni na umaizi vinavyoongoza shughuli zinazoendelea kwenye ngazi ya umma ya jumuiya nzima ya Kibahá'í ulimwenguni, na pia zimenufaika kutokana na ushauri wenye busara wa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na ya Kitaifa.

Tunafurahi kuona sura hizi anuai zenye upatano wa imani inayooneshwa na wafuasi waliojitoa wa Uzuri Uliobarikiwa, katika kuitikia mateso ya ulimwengu uliochanganyikiwa na wenye kufadhaishwa sana.

***Jitihada za Kielimu na taasisi ya mafunzo***

21 Umuhimu wa elimu kwenye dhana ya Kibahá'í ya mabadiliko ya kiroho na kijamii hauwezi kukadiriki hata kidogo "Fikiria", Bahá'u'lláh husema, "ufunuo wa mwangaza wa Jina la Mungu, Muelimishaji. Tazama, jinsi gani shuhuda za ufunuo kama huo zilivyo dhahiri katika vitu vyote, jinsi gani uboreshwaji wa viumbe vyote unavyotegemea juu yake". Umuhimu wa elimu katika kazi ya ujengaji jumuiya ni bayana, na katika uga wa shughuli za kijamii utoaji wa elimu hubakia kuwa utambulisho wa mchango wa Wabahá'í katika sehemu kubwa za ulimwengu. Wa kwanza kabisa miongoni mwa miundo na mawakala walioanzishwa na ulimwengu wa Kibahá'í kwa ajili ya utoaji wa elimu bila shaka ni, taasisi ya mafunzo. Kwa hakika, mtandao wa taasisi za mafunzo za kitaifa na kikanda ukifanya kazi kwa ustadi mkubwa kote ulimwenguni ni miongoni mwa matunda bora kabisa ya mfuatano uliopita wa Mipango ya kiulimwengu. Ujengaji wa uwezo kwa ajili ya huduma ndani ya jumuiya kwa kuiwezesha idadi iongezekayo daima ya watu binafsi kunufaika kutokana na mchakato wa taasisi utaendelea kuwa sura muhimu za Mipango katika mfuatano wa sasa. Uwezo ambao tayari umeibuka kwa ajili ya maendeleo ya jumuiya, ukiwakilishwa na mamia ya maelfu ya watu binafsi ambao wana uwezo wa kuhudumu kama wakufunzi, wahuishaji au walimu wa madarasa ya watoto, ni rasilimali za matokeo ya kihistoria.

22 Tulipoitambulisha dhana ya taasisi kwa mara kwanza, ilikuwa katika mkutadha wa hitaji la kuinua rasilimali watu wa kuchukua kazi za upanuzi na uimarishaji. Kwa wakati huu, ambapo mfululizo wa Mipango mipya ndiyo tu umeanza, tunawaalikeni kuchukua mtazamo upanukao zaidi. Ongezeko la ushiriki kwenye kozi za taasisi ni kuwaandaa marafiki wa Mungu kwa ajili ya ujihusishaji wa kina daima katika maisha ya jumuiya pana zaidi; ni kuwajalia maarifa, umaizi na ujuzi ambavyo huwawezesha kuchangia siyo tu kwenye mchakato wa uendelezaji wa jumuiya yao wenyewe, bali kwenye maendeleo ya jamii. Kwa kifupi, taasisi ni chombo chenye uwezo kwa ajili ya uachiliaji wa nguvu ya Imani ijengayo jamii. Ingawa kazi ya kukuza nyenzo za mtaala ili kusaidia kusudi hili ni jitihada ya muda mrefu, nyenzo zilizopo tayari hulenga kujenga uwezo kwa ajili ya jitihada mbalimbali. Zaidi ya hayo, zinatoa uzoefu wa kielimu uliofumwa na kushikamana pamoja kutoka umri wa miaka mitano, kwenda juu hadi umri wa ujana chipukizi, na hadi kwenye utu uzima, na wanahudumu kama wenzi wa moja kwa moja wa muundo wa shughuli zinazokunjuka kwenye ngazi ya umma. Kuhusiana na hili, tumefurahishwa kuona wingi wa umaizi ambao marafiki katika sehemu mbalimbali za ulimwengu, katika mukutadha wa jamii na tamaduni mbalimbali, wanauzalisha kuhusiana na hali za maendeleo ya jumuiya. Ikiwa umaizi huu, na ule ambao bado haujaibuka, ni wa kunufaisha jumuiya za Kibahá'í kwa mapana zaidi, mifumo kwa ajili ya maandalizi na maboresho ya nyenzo za kielimu itahitaji kupanuliwa. Tukiwa na hili akilini, hivi punde tutatoa mbinu zitakazoongoza kazi hii kwa miaka ijayo.

23 Kuhusiana na ukuzaji wa uwezo wa taasisi kuwasilisha kila mojawapo ya hatua tatu za mchakato wa kielimu, tunayo furaha kuona kwamba umakinifu unaongezeka kutolewa kwenye uimarishaji wa ubora wa tajiriba ya kielimu yenyewe, kama nyongeza kwa upanuzi wa mfumo wa uwasilishaji wake. Hitaji la juu kabisa ni kuwawezesha wale wote wanaochangia kwenye kazi ya taasisi kuendelea kupiga hatua katika uelewa wao wa maudhui ya kielimu: malengo yake, muundo wake, kanuni zake za ufunzaji, mbinu zake, dhana zake kuu, uhusiano wake mbalimbali. Bodi nyingi za taasisi za mafunzo zimesaidiwa kwa namna hii na makundi yanayoshirikiana yaliyoelezwa kwenye ujumbe wetu kwenye kongamano lenu la 2015. Katika maeneo, timu tofauti pia zimeanza kumakinikia kipekee kwenye madarasa ya watoto, vikundi vya vijana chipukizi, na vikundi vya mafunzo, zikibainisha vigezo ambavyo vinachangia kwenye ufanisi wao na kutafuta njia za kuwasaidia marafiki wanaojihusisha katika kila nyanja ya huduma kukuza zaidi uwezo wao wenyewe. Washauri Wasaidizi katika kanda na wasaidizi wao mara nyingi ndiyo wa kwanza kuhakikisha kwamba yale mafunzo yanayopatikana yanaifikia idadi pana zaidi ya marafiki kote ndani ya klasta zinazokaribiana na ndani ya vituo vya shughuli shadidi. Watu binafsi wenye tajiriba ya kina katika kuendeleza shughuli za taasisi wanahudumu kama nguvu kazi, na wamethibitisha kuwa chombo kitumikacho kusaidia taasisi kwenye hatua ya awali ya maendeleo kusonga mbele. Hata hivyo, kwa jumla ni Washauri ambao wanahakikisha kwamba kila taasisi hujifahamisha na umaizi mwingi muhimu unaozalishwa na mawakala wake ndugu katika nchi na kanda jirani. Washauri wamepanga kwa ajili ya taasisi kupangwa kwenye makundi ya ukubwa tofauti tofauti ili kuwezesha masomo yanayofunzwa na taasisi zenye tajiriba zaidi kusambazwa kwa mapana zaidi, kwa kiwango kikubwa kupitia njia za semina rasmi. Mipangilio yote hii itahitaji kuimarishwa wakati wa Mpango ujao. Katika maeneo ambako kituo kwa ajili ya usambazaji wa ujifunzaji kuhusu programu ya uwezeshaji wa kiroho wa vijana chipukizi kinafanya kazi, ushirikiano baina ya kituo cha ujifunzaji na taasisi zihusikazo tayari umethibitisha kuwa wenye manufaa sana, na unapaswa kushadidishwa; utekezaji wao wa lengo la pamoja na shauku yao ya pamoja kuona klasta zinasonga mbele inatengeneza mazingira bora kwa ajili ya moyo wa ushirikiano na kusaidiana vishamiri. Maarifa ambayo sasa yamekusanywa kuhusu vigezo vinavyochangia kwenye ufanisi wa mchakato wa taasisi ni ya kina, na tunatarajia Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa kukusanya mafunzo yaliyopatikana na kuuweka kwa ajili yenu.

24. Tulichokielezea hapo juu ni mfumo wa kielimu ambao upo katika hali ya kuboreshwa daima. Hili linawahitaji watu binafsi wengi kuunga mkono maendeleo yake zaidi, pia linahitaji taasisi, na Asasi za Kibahá'í kwa jumla zaidi, kufanya mipango mapema na kuhakikisha kwamba watu binafsi ambao wamekuza uwezo wa kutosha katika kusaidia jitihada za kielimu za jumuiya wanaweza kudumisha huduma yao na wanaweza, wakati hali zao za maisha zinapobadilika, kuendendelea kujihusisha katika kazi ya taasisi kwa njia zingine zenye maana. Kwa kuthamini ufanisi wa mchakato wa taasisi, kila mfuasi wa Bahá'u'lláh atahisi shauku ya kuchangia kwenye ukuaji wake kwa namna fulani—bila kuwaacha vijana wa Kibahá'í. Taasisi zinajua fika kuwa uachiliaji wa uwezo uliomo ndani ya vijana, ni jukumu takatifu; sasa tunaomba kwamba vijana wa Kibahá'í waangalie maendeleo ya taasisi ya siku zijazo katika mwanga ule ule mmoja. Katika uanzaji wa miaka tisa, jitihada pana ya jumuiya kuileta taasisi

kwenye kiwango cha juu cha utendaji, tunatarajia kuona mjongeo mpana wa vijana wakiweka kigezo. Sharti wachukue kila fursa—katika shule zao na vyuo vikuu, na katika nafasi zilizo maalum kwa kazi, familia au mchangamano wa kijamii—kutia moyo roho nyingi zaidi na zaidi kunufaika kutokana na programu za taasisi. Baadhi ya vijana wataweza kujitolea kipindi cha huduma—huenda hata kwa miaka mfululizo—kwa ajili ya utoaji wa elimu, hususan kwa wale ambao ni wadogo zaidi kuliko wao wenyewe; kwani kwa wengi, usaidizi kwenye shughuli za taasisi utakuwa sehemu ambayo daima ipo katika maisha yao katika kipindi chote cha elimu yao na kadiri wanavyotafuta riziki kutokana na mwito wao katika ulimwengu huu; lakini isiwe kwa yeyote kuchukulia kwamba ni kitu kingine chochote zaidi ya shangwe ya kujitoa kwao.

25 Katika maeneo mengi ya ulimwengu, matokeo ya kawaida ya ushiriki wa watu binafsi na familia katika mchakato wa taasisi yamekuwa ni utambuzi uongezekao wa umuhimu wa elimu katika sura zake zote. Marafiki wanaohudumu kama walimu wa madarasa ya watoto wanaweka mkazo wa kina katika maendeleo mapana ya kielimu ya wale wanaowafundisha, wakati marafiki wanaohudumu kama wakufunzi na wahuishaji kwa kawaida wanajali kiwango ambacho wale ambao wanakaribia au wanaingia utu uzima—wasichana kwa wavulana kadhalika—wanaweza kukifikia na kunufaika kutokana na elimu ya aina mbalimbali, siyo tu kwa ile inayotolewa na taasisi yenyewe. Mathalani, wanaweza kuwatia moyo vijana kujikita katika ufundi au mafunzo ya chuo kikuu. Tumeshangazwa na namna, katika jumuiya nyingi, ujihusishaji wa idadi kubwa katika mchakato wa tasisi ulivyobadilisha pole pole hali hii ya utamduni ndani ya jamii ya watu. Asasi za Imani zitahitaji kuchukua jukumu kwa kuhakikisha kwamba, kadiri ufahamu unavyoinuliwa katika njia hii, matarajio bora ambayo yanaibuka ndani ya vijana kama matokeo—matarajio ya kupata elimu na mafunzo ambayo yatawaruhusu kutoa huduma ya maana kwa maisha yote kwa jamii zao—yataweza kutimizwa. Maendeleo ya muda mrefu ya jumuiya na, hatimaye, ya taifa, kutoka kizazi hadi kizazi, hutegemea kwa sehemu kubwa juu ya jitihada zilizofanywa za kuwekeza katika wale watakaochukua jukumu kwa ajili ya maendeleo ya pamoja ya kijamii.

26. Utafiti huu wa umuhimu wa elimu kwa jumuiya unaoasisiwa juu ya kanuni za Kibahá'í usingekamilika bila uchunguzi zaidi. Shoghi Effendi ameweka msisitizo mkubwa juu ya umuhimu wa kujitahidi, kupitia "jitihada endelevu", kupata "uelewa wa kutosha zaidi wa umuhimu wa Ufunuo wa ajabu wa Bahá'u'lláh". Taasisi ya mafunzo haina kingine inachofanana nacho kama chombo cha kufunulia idadi isiyo na kikomo ya roho, maji Ufunuo yatiayo uzima na maana zisizoisha za Neno la Mungu. Lakini jitihada za marafiki za kuongeza uelewa wa Imani na mafundisho yake bila shaka hazikomei kwenye ushiriki katika mchakato wa taasisi. Kwa hakika kiashirio kimojawapo chenye nguvu cha ufanisi wa taasisi ni kiu inayoisababisha ndani mwa wale wanaojihusisha na nyenzo zake kuendelea kujifunza Hoja ya Bahá'u'lláh—kama mtu binafsi, lakini pia kwa pamoja, iwe katika nafasi rasmi zilizoandaliwa na asasi au katika mazingira yasiyo rasmi zaidi. Mbali na kujifunza Ufunuo wenyewe, athari ambazo mafundisho hubeba kwa nyanja zisizohesabika za jitihada za kibinadamu ni zenye umuhimu mkubwa. Mfano mmoja utambulikao wa aina mojawapo ya elimu ambayo kupitia humo waumini vijana wanapata ufahamivu mzuri zaidi wa mtazamo wa Kibahá'í kwenye masuala yanayohusiana na maendeleo ya jamii ya binadamu ni

ushiriki katika semina zinazotolewa na Taasisi ya Masomo kwa Ustawi wa Ulimwengu. Ukichukulia ukubwa wa bahari ya Ufunuo, itakuwa dhahiri kwamba kuvitafiti vina vyake ni kazi ya maisha yote ya kila roho ambayo ingetembea njia ya huduma.

27 Kadiri mchango unaofanywa na Imani kwa maendeleo ya jamii katika sehemu mbalimbali za ulimwengu unavyopata muonekana mkubwa zaidi, jumuiya ya Kibahà'i itaendelea kuitwa zaidi kufafanua kwa undani kanuni inazozitetea, na kuonesha utumikaji wake katika masuala yanayoikabili jamii ya binadamu. Kadiri maisha ya kiakili ya jumuiya yanavyochanua na kushamiri zaidi, ndivyo unavyokuwa mkubwa zaidi uwezo wake kujibu wito huu. Itakuwa ni juu ya wafuasi wa Bahá'u'lláh kutoa, katika ulimwengu wa mawazo, msimamo wa kiakili na uwazi wa mawazo ili kuoanisha kujitolea kwao kwa ajili ya maendeleo ya kiroho na ya kimwili katika ulimwengu wa vitendo.

***Kukuza uwezo kwa ajili ya utawala kwenye ngazi zote***

28. Miaka themanini iliyopita, barua iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi ilielezea Utawala wa Kibahá'í kama "uundwaji wa kwanza wa kile ambacho katika siku zijazo kitakuja kuwa ndiyo maisha ya kijamii na sheria za maisha ya jumuiya". Leo, mwanzoni mwa karne ya pili ya Zama za Ujenzi, umbo la Utawala wa Kibahá'í limekua kwa kiasi kikubwa, na ukuaji wake endelevu utakuwa muhimu kwa ajili ya uachiliaji wa nguvu ya Imani ya ujengaji jamii.

29 Utawala wa Imani kwenye ngazi ya umma, bila shaka, umeunganika kwa karibu sana na ukuaji wa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali. Nyumba hizi changa za Haki zimeelezewa na Shoghi Effendi kama "mishipa mikuu ya jamii ya Kibahá'í, hali kadhalika msingi mkuu wa muundo wake wa kiutawala", na anasisitiza kwa kiasi kikubwa juu ya umuhimu wa uundwaji wake. Mnamo 1995, tulitoa wito wa kurejeshwa kwa desturi iliyohitaji Mabaraza yote ya Mahali, yakiwemo yale mapya yanayoundwa, kuchaguliwa Siku ya Kwanza ya Riḍván badala ya wakati mwingine wowote wa mwaka. Ukuaji huu ulihusiana na ukweli kwamba, wakati waumini kutoka nje ya eneo moja wangeweza kusaidia mchakato wa uchaguzi, jukumu la kimsingi kwa ajili ya kuchagua Baraza lolote na kudumisha shughuli zake linabakia mikononi mwa Wabahá'í wa eneo hilo; zaidi hutegemea juu ya utayari wao kwa ajili ya kuchukua shughuli za kiutawala. Katika miaka ya hivi karibuni, imeonekana jinsi gani dhana ya utambulisho wa Kibahá'í pole pole inavyoweza kupata nguvu katika eneo moja kadiri mtindo wa utendaji uliojikita katika mafundisho unavyozoeleka miongoni mwa watu binafsi na familia zinazoishi hapo. Hivyo, jumuiya mara nyingi itakuwa imefikia kiwango fulani cha uwezo kuhusiana na jitihadi za ujengaji wa jumuiya kufikia wakati wa uundwaji wa Baraza la Mahali unapowezekana. Kadiri hatua hii inavyokaribia—na haipaswi kucheleweshwa bila sababu—jitihada lazima zifanyike kukuza uthamini wa sura rasmi za maisha ya jumuiya zinazohusiana na utawala wa Kibahá'í. Baraza la Mahali linaloibuka katika mazingira kama hayo lina uwezekano mkubwa wa kutambua jukumu lake la kuhamasisha na kuimarisha zile shughuli zitakazosaidia kudumisha jumuiya hai. Hata hivyo, pia litahitaji kupata umahiri katika kutekeleza safu pana zaidi ya majukumu mengine, na usaidizi unaotolewa na wasaidizi wenu pamoja na wasaidizi wao kwake utakuwa wenye umuhimu mkubwa. Katika ujumbe wetu kwa kongamano

lenu la 2010, tulielezea njia ya kiukuaji ya Baraza kama hilo, na tulirejelea kwenye sura mbalimbali za utendaji wake ambazo zingehitaji kupewa umakinifu, ikiwemo ni pamoja na uwezo wake kusimamia na kukuza Hazina ya Mahali na, kwa wakati, kusaidia jitihada za shughuli za kijamii na kuchangamana na mawakala wa serikali za mitaa na asasi za kiraia. Manufaa yanayopatikana kwa jumuiya inayohudumiwa na Baraza kama hilo hayahitaji ufafanuzi.

30. Katika mchangamano wenu na Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa pamoja na Halmashauri za Kibahá'í za Kanda, tunaomba kwamba muweke umakini juu ya suala la uanzishwaji wa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na kuimarisha shughuli zao, hususan katika maeneo ambako sura hii ya ukuaji inaweza kuwa imepokea mkazo mdogo. Tunatarajia hili litachangia kwenye ukuaji wa haraka wa idadi ya Mabaraza ya Mahali yatakayoundwa mwaka hadi mwaka. Katika baadhi ya nchi, ushauriano wenu utahitaji kujumuisha kuangalia ikiwa katika maeneo ya vijijini mipangilio iliyopo ya kubaini mipaka ya kila eneo inatosheleza.

31. Umaizi mmoja ushurutishao ambao umeibuka ni kwamba kiwango ambacho kwacho daraja na uongozi wa Baraza la Mahali vinatambulika katika jumuiya kinahusiana na jinsi waumini wanavyothamini kwa kina utakatifu wa mchakato wa uchaguzi na wajibu wao wa kuushiriki, katika mazingira ambayo ni huru kabisa kutokana na dosari ya ushawishi au mitazamo ya kidunia kuhusu madaraka. Wakati utambuzi umeinuliwa katika jumuiya kuhusu kanuni za kiroho zinazosimamia chaguzi za Kibahá'í, dhana mpya inaundwa ya kile kinachomaanishwa kwa mtu kuitwa kuhudumu katika asasi, na ufahamu huongezeka wa jinsi mtu binafsi, jumuiya, Baraza la Mahali na mawakala wake wanavyohusiana mmoja kwa mwingine. Pale ambapo juhudi zenye mpangilio zimefanywa kuchochea mazungumzo katika jumuiya kuhusu uundwaji wa Baraza la Mahali na kusudi lake, na kudumisha mazungumzo hayo mwaka hadi mwaka, uimara wa chombo kilichochaguliwa na nguvu ya maisha ya jumuiya huimarishana.

32 Matokeo haya ya kukubaliana yameonekana dhahiri hususan ndani ya kipindi cha miaka miwili iliyopita katika maeneo ambayo tumeridhia utumiaji wa hatua mbili za mchakato wa uchaguzi kwa ajili ya Baraza la Kiroho la Mahali, mbinu ambayo chimbuko lake limo katika maagizo yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá kwa Baraza la Kiroho la Ṭehrán. Mabaraza ishirini na mbili ya Mahali, yaliyosambaa katika nchi nane, tayari yameanza kuchaguliwa kwa njia hii katika kipindi hiki. Ukifanana na uchaguzi wa Baraza la Kiroho la Kitaifa kwa namna nyingi, huhusisha mgawanyo wa eneo katika maeneo madogo madogo zaidi (unit) ambayo kutoka kila moja ya hayo mwakilishi mmoja au zaidi huchaguliwa, ambapo baada yake wawakilishi hawa huchagua wajumbe wa Baraza la Mahali. Kadiri idadi ya Wabahá'í wanaoishi ndani ya eneo inavyoendelea kupanuka na uwezo wa jumuiya kusimamia utata unavyoongezeka, suala la utekelezaji wa hatua mbili za mchakato wa uchaguzi huwa ni kipimo chenye nguvu zaidi. Kulingana na hilo, katika Mpango ujao, tunatarajia kuidhinisha utumiaji wa njia hii kwa ajili ya kuchagua Baraza la Mahali katika maeneo mengi zaidi, kote mijini na vijijini, ambako hali hufanya hatua kama hii ya wakati muafaka.

33. Baraza la Kiroho la Mahali hudumisha umakini wa kina katika kujifunza namna nzuri zaidi ya kuendeleza kazi ya ujenzi wa jumuiya ndani ya eneo la mamlaka yake, na hivyo hushauriana mara kwa mara na marafiki wanaohusika katika kuratibu jitihada ndani ya klasta. Hufuatilia kwa karibu maendeleo ya vituo vyovyote vya shughuli shadidi ndani ya eneo, hususan kwa kutoa msaada kwa timu za waumini ambao wameibuka humo na wanachochea mchakato wa ukuaji. Kwa jumla, kadiri shughuli zinavyozidi kushadidishwa huhitaji mipangilio ya kiutaratibu kwenye ngazi ya eneo au katika baadhi ya sehemu za eneo—tuseme, kupangilia kampeni za ziara za majumbani, kuambatana na familia zinazokaribisha mikutano ya ibada, au kuwatia moyo kuunda vikundi vya kufanya kazi pamoja—ndivyo jukumu linaloweza kutwaliwa na Baraza la Mahali kuhusiana na hili linavyozidi kujitokeza zaidi. Katika maeneo ambamo idadi kubwa ya watu inakaribishwa kukumbatia shughuli za Kibahá'í, na pale ambapo utata wa kazi ya Baraza na majukumu mengi yanapoongezeka, Baraza wakati mwingine huona kwamba Katibu wake huhitaji kusaidiwa na ofisi yenye wafanyakazi, na hatimaye, haja kwa ajili ya kuwa na Ḥaẓíratu'l Quds stahiki ya Mahali huwa ya haraka zaidi.

34. Kadiri Mabaraza ya Mahali yanavyoanza kutwaa sehemu kubwa zaidi na zaidi ya majukumu kwa ajili ya kulea maendeleo ya jumuiya, asasi kwenye ngazi za kanda na kitaifa lazima ziwe zenye mpangilio zaidi katika juhudi zao za kuwasaidia. Tumefurahishwa kuona hitaji hili likishughulikiwa kiutaratibu, mathalani kupitia Mabaraza ya Kitaifa au Halmashauri za Kanda kuitisha mikutano ya mara kwa mara na Makatibu na maafisa wengine wa Mabaraza ya Mahali kwa ajili ya kushauriana kuhusu ukunjukaji wa njia mahususi za kiutendaji.

35. Pale ambapo Halmashauri ya Kanda imekuza uwezo ulioimarishwa kwa ajili ya utawala, ukiwemo uwezo wa kutoa aina zifaazo za msaada kwa klasta nyingi kwa wakati mmoja, hii imekuwa ya kufaa kwenye mchakato uliochapuzwa wa kanda nzima. Ujumbe wetu kwa kongamano lenu la mwaka 2015 ulionesha kuwa katika nchi ndogo zaidi ambamo uanzishwaji wa Halmashauri za Kanda hauhitajiki, muundo rasmi ungehitaji kuibuka kwenye ngazi ya kitaifa ambao ungepewa wajibu wa kuzisaidia klasta kusonga mbele. Tunaomba kwamba, katika nchi ambako hili bado halijatokea, ninyi sasa mshauriane pamoja na Mabaraza ya Kitaifa kuhusu hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa ajili ya kuteua chombo rasmi, yaani, Kamati ya Ukuaji ya Kitaifa yenye wajumbe watatu, watano, au saba. Baraza la Kitaifa litahitaji kumpa wakala huyu nafasi ihitajikayo ya kukuza mjongeo wa klasta, akichota umaizi ufaao kutokana na ule ujifunzaji uliopatikana kuhusu Halmashauri za Kanda kuhusiana na hili. Majukumu yake yanaweza kujumuisha kuteua Kamati za Ufundishaji za Eneo na kuzihamasisha katika mipango yao, kufanya maandalizi ya kutuma watangulizi wa ndani, kusaidia miradi ya ufundishaji na kusambaza vitabu vya kimsingi. Kamati hii itafaidika kutokana na uwezo wa kushirikiana kwa karibu na taasisi ya mafunzo, yenyewe ikiwa wakala wa Baraza la Kitaifa, na pamoja na Washauri Wasaidizi wanaohudumia nchi, na vile vile itaweza kuwasiliana moja kwa moja na Mshauri husika. Wakati Baraza la Kitaifa kwa kawaida litapenda kudumisha ufahamivu endelevu wa kazi za Kamati na kuipatia miongozo, msaada na hamasa, uundaji wa chombo ambacho hujishughulisha kikamilifu na uendelezaji ukuaji sharti kuliwezeshe Baraza kumakinikia zaidi masuala mengine

muhimu. Katika nchi ambako Halmashauri hazijaundwa lakini hatimaye zingeweza kuanzishwa, Kamati ya Ukuaji ya Kitaifa pia inapaswa kuteuliwa wakati huu.

36. Kadiri nguvu za kiroho zinazoachiliwa kupitia utekelezaji wa dhati wa Mpango zinavyojimwaga, zinakutana na upinzani kutoka nguvu kinzani zinazoizuia jamii ya wanadamu kufikia ukomavu wake kamili. Mbele ya nguvu kama hizo, uwezo hai wa njia mbalimbali za kiutendaji zinazofuatwa kwenye ngazi ya mahali zinahitaji kuhifadhiwa na kuimarishwa. Jukumu hili tunduizi ni lenye umuhimu maalum kwa wajumbe wa Bodi mbili za Wasaidizi, ambazo majukumu yao mengi, nyeti huwaunganisha kwa ukaribu na hali zilizopo kwenye ngazi ya umma na huhadharisha kwa chochote kinachoweza kuathiri hali ya kiroho ya jumuiya. Katika tamaduni na mazingira tofauti tofauti ya kijamii kote, lazima wawasaidie marafiki kukabiliana na changamoto za aina mbalimbali: kuvisaidia vikundi ambavyo awali vilikuwa na ushindani kupata umoja kupitia utekelezaji wa lengo moja; kujifunza kuziweka kando desturi za kurithi na mielekeo ambavyo ni sehemu ya kipindi cha ujana wa jamii ya binadamu, na kuzishinda chuki za aina zote; kujihadhari dhidi ya muelekeo wowote wa kutazama mambo kwa kebehi au kwa jicho la ukosoaji, na badala yake kudumisha mtazamo wenye shauku na unaojenga; kuweka usawa wa wanawake na wanaume katika vitendo; kuondokana na utepetevu na uzembe kupitia jitihada binafsi, kutanguliza usaidizi binafsi wa mipango kwa ajili ya utendaji wa pamoja badala ya hisia za upendeleo wa mtu binafsi; kutumia nguvu ya teknolojia za kisasa bila kukubali kuathiriwa na athari zao; kuthamini utamu wa kufundisha Imani na furaha ya kuihudumia jamii ya binadamu dhidi ya raghba za kidunia; kukataa kuleweshwa na ulafi; na kuzipa kisogo fikra za kiyakinifu na mtazamo wa kiulimwengu unaokuzwa nazo, na kukazia macho kwenye taa angavu ambayo ni sheria na kanuni za Mungu. Hizi, na zingine nyingi kando yake, huunda seti yenye nguvu ya majukumu kwa ajili ya utekelezaji wa kikosi cha waaminifu wakati wanavyopitia yale ambayo kwa hakika yatakuwa miaka ya mihangaiko katika maisha ya jamii ya wanadamu. Wasaidizi wenu, ambao wamejipatia sifa sana katika kuendeleza mchakato wa uingiaji kwa makundi, lazima waende sawa katika kukabiliana na changamoto kama hizo wakati wowote na popote zinapojitokeza. Kupitia nguvu ya mfano wao mzuri na ufasaha wa ushauri wao mzuri, hebu na wawasaidie marafiki kukua katika imani, uhakika na kujitoa kwa maisha ya huduma, na kuambatana nao wakati wanapojenga jumuiya ambazo ni makao ya amani, mahali ambako jamii ya wanadamu iliyosumbuliwa na yenye makovu ya migogoro inaweza kupata hifadhi.

37. Kwenye mfuatano uliopita wa Mipango, uwezo wa jumuiya kudumisha mkazo juu ya mahitaji ya lazima sana ya Imani uliibuka kama mojawapi ya nguvu yake muhimu kabisa. Hata hivyo, hisia hii ya mkazo haina budi kujumuisha njia nyingi za kiutendaji, ambapo zote sharti zisonge mbele bila kuwa katika ushindani. Hili linahitaji maono yaliyopanuliwa, uelewa wa kina wa vipengele muhimu vilivyopo, unyumbulifu wa ziada na ushirikiano wa hali ya juu kabisa wa kiasasi. Tunatambua kwamba rasilimali za Imani zina kikomo, na watu binafsi huhisi kukabiliwa na mahitaji mengi juu ya muda wao. Lakini kadiri Mpango unavyokunjuka katika sehemu moja na safu za wale walio tayari kuhudumu zinavyoongezeka, sura mbalimbali za maisha yaliyoshamiri na yenye uhai ya jumuiya ya Kibahá'í zitapiga hatua, na nguvu ya Imani ya ujengaji jamii itang'ara.

***Dhima ya kihistoria***

38. Tunatumaini tumewafurahisha, katika kurasa hizi, kwamba uwezo wa wakati huu wa jumuiya ya Kibahá'í, ukichanganywa na nidhamu iliyojipatia kupitia uzingatiaji wa muundo madhubuti wa utendaji, umeiandaa kwa ajili ya jaribio kubwa, kali la rasilimali zake zote, za kiroho hali kadhalika za kimwili. Mpango ambao utaanza hivi karibuni— mradi mkubwa wa kwanza kufanyika katika shughuli takatifu ya miaka ishirini na tano, wa vizazi katika ukubwa na umuhimu wake—utaweka uhitaji wa muumini binafsi, jumuiya na asasi, unaofanana na uhitaji ambao Mlinzi aliufanya kwa ulimwengu wa Kibahá'í mwanzoni mwa Mpambano wa Miaka Kumi. Kama, kwa neema ya Mwenyezi Mungu, marafiki wakifanikiwa kuvifikia vilele vya ushujaa ambavyo kwavyo sasa wanaitiwa, kwa hakika historia itavienzi vitendo vyao kwa namna ambayo si pungufu kwa mng'ao kuliko ile ambayo hutumika kuvienzi vitendo vitukufu ambavyo huiremba kumbukumbu za kihistoria za karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi.

39. Tunaweka tegemeo kubwa juu yenu na juu ya Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa kuhakikisha kwamba, katika juhudi zote zinazofanywa kuwafahamisha marafiki asili ya shughuli hii ya pamoja, mtazamo wa historia unawekwa machoni kikamilifu. Ustaarabu wa leo, pamoja na uwezo wake wa kimali, umekutwa kuwa wenye kasoro, na hukumu imetolewa na Kalamu Kuu Kabisa: "Hamjui kwamba Tumekikunja kile ambacho watu walikimiliki, na badala yake tumekunjua utaratibu mpya?" Uanzishwaji wa Ustaarabu Mtakatifu, katika maneno ya Mlinzi, ni "dhima ya msingi ya Imani ya Kibahá'í". Unapaswa ujengwe juu ya sifa za kimsingi kabisa, zile ambazo ulimwengu unazihitaji sana: umoja, uaminifu, kusaidiana, ushirikiano, hisia za urafiki, kutojipendelea nafsi, kujifunga katika ukweli, hisia ya uwajibikaji, kiu ya kujifunza, upendo wa moyo ukumbatiao vyote.

40. Jinsi gani tunatamani kuiona jamii ya binadamu ikiangaziwa kwa upendo wa Bwana wake; jinsi gani tunatamani kusikia sifa Zake kwenye kila ulimi. Mkifahamu shauku ya tamanio letu, mnajua basi hisia ambayo kwayo, tukiweka vichwa vyetu juu ya Kizingiti Kitakatifu Kabisa, tunamsihi Bahá'u'lláh awafanye ninyi, na wote ambao huipenda Imani Yake ya thamani, daima kuwa mifereji kamili ya neema Yake isiyoelezeka.

[Imesainiwa: Nyumba ya Haki ya Ulimwengu]